# DHAMIRA ZA KIJIJI CHETU

*Zacharia Mochiwa*

Ngalimecha Ngahyoma amejitoma katika uandishi wa tamthiliya kwa mara ya kwanza alipotuletea jukwaani matatizo ya mabinti katika *Huka.* Kwa hiyo sitokuwa nimekosea kwa kusema sasa msanii huyu anaanza kuuzoea uwanja huu. Ama Ngahyoma amejitoa mhanga kujadili matatizo ya jamii kwa kutumia jukwaa na si jukwaa la hivi tu bali jukwaa ambalo limetanguliwa na utafiti thabiti wa matatizo ya jamii yake kuonyesha kuwa vituko vilivyomo katika tamthiliya ya *Kijiji Chetu* vilitokea au vinatokea. Katika utangulizi wake Ngahyoma anasema: Baadhi ya mambo niliyoyachunguza katika vijiji vya ujamaa yamebadilika. Shida au matatizo yamerekebishwa..." Hali kadhalika hoja ya utafiti inajidhihirisha katika utangulizi huo huo alipotoa shukrani kwa "ndugu wanavijiji nilivyotembelea kwa mawazo na mazungumzo ya kidugu na ushirikiano wao na hata kufanya mchezo huu kuwa katika hali hii."

Vijiji vya Ujamaa katika Tanzania ni nguzo kuu ya Ujamaa. Ni msingi wa siasa yetu ya Ujamaa na Kujitegemea na tunaweza kusema kuwa vijiji hivi ni moyo hasa wa siasa yetu. Kufanikiwa kwa vijiji vya Ujamaa ni kufanikiwa kwa siasa yenyewe. Aidha kuzorota kwavyo ni kuzorota kwa maendeleo ya nchi. Kutokana na kumaizi umuhimu huu wa vijiji kwa kutumia tamthiliya ya *Kijiji Chetu,* Ngahyoma anasema kwamba vijiji vya ujamaa vina matatizo mengi na miongoni mwayo ni uongozi, uvivu, ujamaa na ndoa.

## 1. UONGOZI

Katika vijiji sasa hivi kuna tatizo la uongozi. Jambo lolote lile haliwezi kufanikiwa bila na kuwa na uongozi thabiti, uongozi wa watu au tuseme uongozi bora. Uongozi bora ni ule unaohakikisha kuwa yale yanayoamuliwa na umma yanatekelezwa. Ni uongozi unaolinda uamuzi wa pamoja wa mambo yote yanayohusu kijiji. Lakini kwa bahati mbaya viongozi wa vijiji bado hawajapevuka kifikra ndiyo maana twapata kauli kama hizi:-

> *MTU 1:* Maendeleo ya kijiji chetu ni mazuri kwa upande wa vitu. Lakini upande wa mawazo ya kijamaa kwa kweli bado... Mawazo yetu yanatazama utajiri wa binafsi na hii inadhihirishwa na vitendo vya viongozi wetu... Kwa kutumia njia za ulaghai, uhaini na unyonyaji wanatunga njia za kuwawezesha kupata faida kubwa ya vitu na matunda ya jasho letu...

Pamoja na kujinufaisha huko viongozi wanajitafutia enzi, uwezo na utukufu. Katika hima hiyo viongozi wanawanyanyasa wananchi wengine na kutumia madaraka yao kwa kuwatia ndani wasithubutu tena kuchezea wenye mamlaka.

*PINDUO:* Ni hivi karibuni tu kitendo cha kiongozi fulani kimedhihirisha uonevu tunaofanyiwa. Tulikuwa tumeketi kwenye baa yetu tukinywa tukifurahi wakati mkuu fulani alipofika na rafiki yake na kuagiza pombe. Kama wote tunavyofahamu, magilasi tunayatoa kwa wakati maalum tu. Lakini mwenzetu kwa siku hiyo akakataa kupiga tarumbeta, akadai apewe gilasi. Kwa utani tu kijana mmoja alimjibu kuwa gilasi lake liko nyumbani kwake. Bwana akaja juu, 'Umenidharau na kunivunjia heshima... oh umenitukana' Akamwita askari na kijana akawekwa ndani. (uk. 20)

Aina hii ya uongozi ni ile inayosisitiza kuwa kiongozi ni mtu mkubwa, mstahiki na hana nafasi ya kufanyiwa mzaha. Kiongozi huyu huhakikisha kuwa anajibari na watu ili wasimzoee halafu wakamdharau wasije kuvunja amri zake, maana mazoea huleta dharau! Kwa vyovyote vile mtu ambaye hukumzoea akikupa amri utaitekeleza haraka haraka si kwa kuwa umekiri uongozi wake bali kwa kuitafuta heri yako. Huu ndio uongozi unaomfanya Kizito alalamike kama hivi:

*KIZITO:* Sikuja hapa kulazimishwa kufanya kazi. Sikuja hapa kupangiwa kazi kama askari. Kwa nini wao wenyewe wasije kulima! Nani asiyetaka kukaa ofisini! Kama wanataka usawa, wote tulime na wote tukae ofisini. (uk. 6).

Hatuwezi kuyachukua maneno haya ya Kizito juu juu tu bali katika undani wake tuichukue fikra moja kubwa kwamba uongozi umeshindwa kuwashirikisha wananchi katika kutoa uamuzi. Hali hii imesababisha watu kama Kizito kufikiri kuwa maadam wao ni viongozi wasingeweza kujitupa juani kwa hivyo wamejiweka ofisini ilihali wale wasio na satua wanaungua juani. Basi ingawa ni kweli kuwa kuna mgawanyo wa kazi katika kijiji lakini nani mwenye madaraka ya kutoa mgawanyo huo; ni wanakijiji wote au watu fulani tu? Maana uenyekiti si uamirijeshi wa kijiji. Wanakijiji ni watu huru na kazi ya Mwenyekiti ni kuhakikisha kuwa uhuru huo wa watu haupotei.

Ikiwa uongozi ni kioo cha matarajio ya wanakijiji katika kufikia lengo letu la Ujamaa, viongozi wa *Kijiji Chetu* hawana nuru hiyo. Viongozi wanaitumia wadhifa hii kwa kukidhi haja zao na tamaa zao za kulimbikiza mali. Tabia hii inavunja moyo wanakijiji. Kwa bahati mbaya wanavijiji wetu wengi hutetea kweli tamu tu kwa viongozi. Ni wachache walio shupavu kiasi cha kumkabili kiongozi kwa kusema ukweli kama alivyofanya Kizito.

*PINDUO:* Kama kusema kuwa Bwana Mwenyekiti amefuga kuku wengi kinyume cha maazimio ya kijiji ni uwongo basi ndugu wanakijiji mnaweza kuniadhibu... Lakini heri ya uvivu wangu kuliko miiko inayofanywa na Mwenyekiti... Duka lake linalouzwa na mke wake hupata vitu kutoka wapi? (uk. 39—40).

Tabia hii haikuzuka hivi hivi tu bali imetokana na tabia ya viongozi ya kuwasakama wananchi ambao wanathubutu kuusema huo ukweli. Pinduo hafukuzwi katika kijiji kwa uvivu bali kwa kuwa anasemekana kuwa ni mtu ''hatari sana.''

*MTU 2:* Pinduo ndugu ni mtu hatari zaidi kuliko Kizito. Mnamwona siku hizi anavyopita kutongoza watu kila nyumba kupanda mbegu za uasi. (uk. 16)

Je huyu Pinduo ni mtu hatari kwa kina nani hasa? Pinduo anaandamwa kwa kuwa ameamua kusema ukweli. Tunajiuliza; kwani kusema ukweli ni makosa? Au kwa kutumia elimu na ujuzi wake ni makosa? Tunamsikia mwenyewe Pinduo akisema.ndugu elimu haizeeki. Hakuna ubaya mtu kujiongezea kajielimu kengine kadogo." (uk. 19).

Katika kuthibitisha sababu ya kufukuzwa kwake tunaambiwa hivi:

*MTU 1:* Na bado hujanifahamu vizuri. Hebu tujiulize kwa nini Pinduo mtu ambaye alikuwa mwanamapinduzi halisi na mpaka sasa naweza kumwita hivyo, kabadili mwenendo wake! Alipofika hakuwa kiongozi wetu katika kikundi hiki? Hakuwahi kutunukiwa heshima ya mwanakijiji bora wa mwaka!... Siyo wote wenye moyo kama Pinduo. Pinduo humwambia mtu kweli yake mbele ya uso. Ni bora kuliko uzabizabina. Wengi tunajidai tu wazuri lakini uzuri wetu ni kama yai viza, wengi wetu waoga. Huo ndio ukweli wenyewe. Tunamchukia Pinduo kwa yake anayotuambia. Anayowaambia viongozi..." (uk. 16)

Kwa hali ya maendeleo ilivyo sasa hivi ni juu ya viongozi kujifunua mioyo yao na kuwasogelea wananchi ili ushirikiano wa dhati upatikane. Maana ingawa maagano yapo kama methali ya Kizigua isemavyo, "maagano ni maagano mwanasimba hali mbaa," lakini uso wa simba bado wamtisha mbaa!

2. UVIVU

Ngahyoma ametudhihirishia tatizo la uvivu katika vijiji vyetu. Ama tatizo hili kama la uongozi si la vijiji tu bali sehemu karibu zote katika nchi yetu sasa hivi zinaugua taabani kwa ugonjwa huu. Watu wengi wamejifunza kuzungumza "Kichama" lakini bado hawajajua au tuseme hawajaamua kutenda "Kichama." Ngahyoma anaonyesha kuwa, kuna watu ambao wanatega kazi na halafu wanatarajia kupata haki sawa na wale ambao wamefanya kazi kwa kufuata utaratibu na kanuni zilizowekwa. Jambo hili pamoja na kueleweka, Linawaingiza wanakijiji katika mjadala mkubwa na wanaulizana: "Tuwafanyeje watu hawa?" Kwa bahati mbaya mpaka sasa wanakijiji hawajajua la kufanya. Kuna wale ambao wanafikiri dawa ni kuwafukuza.

*MTU 2:* Hakuna sababu ya kuwaweka katika kijiji chetu. Wengine tuwe tunatoa jasho wao wawe wanachonga midomo tu. Hata kidogo ndugu. Watu wa namna hii waende. Hawana nafasi katika kijiji chetu.

*SAUTI:* (Makelele). Sawaa - Pasua. - Waondoke ... (uk. 9).

Ufumbuzi huu pengine ungeweza kuwa dawa kwa watumishi wa kuajiriwa lakini si kwa wanakijiji wavivu. Maana waajiriwa wanapofukuzwa makazini kwao hurejea kijijini kukaa na wazazi na ndugu zao, lakini kuwafukuza wanakijiji wavivu kutoka kijijini ni kuwatoa na kuwaweka mbali na wazazi na ndugu zao; kwa kifupi kuwatenga na jamii zao. Waende wapi?

*MZEE 1:* Kijiji si peponi ambako hakukosi watu wabaya. Hatuwezi kuwa wote wazuri. Jambo la kufanya ni kuwatafutia dawa. Labda wengine mnaweza kupendekeza njia itakayofaa lakini si kuwafukuza... Mnataka tuwafukuze, waende wapi? Kijiji sasa kimekuwa nyumba na maskani yao. Kimekuwa kama

mama mlezi na watoto wake. Kama watoto wamekosa je mama au baba atawafukuza watoto kutoka nyumbani? Watakimbilia wapi? Hapa ni kwao na maisha yao yatabaki kuwa hapa. Mkiwafukuza tutakuwa tumepiga hatua kumi nyuma. Tujitahidi kuwarekebisha waone wajibu wao katika kijiji. Kitu ni kuvumiliana. Tusilete uadui ndani yetu. (uk. 14)

Ni kweli kwamba kuwafukuza si jawabu ya tatizo lakini shida iliyopo ni kwamba watarekebishwa vipi. Maana uvivu waweza kuwa tabia na tabia si rahisi kurekebika, ndiyo maana wengine wakasema tabia haina dawa mpaka ijiague yenyewe. Aidha baadhi kubwa ya wavivu hawa walikuwa wazururaji mijini kwa siku nyingi sana. Kuja kwao vijijini ni kutokana na fukuto walilotiwa na Serikali hadi wakashindwa kupumua au shida ziliwazonga mno mjini ndipo wakaamua kurudi kijijini.

*RIZIKI:* Lakini Kizito, wewe umekuwa rafiki yangu mkubwa siku nyingi toka tutoke mjini. Na naona urafiki huu tusiuharibu na sidhani kama nikijaribu kukushauri, kukushauri kama rafiki yangu utaniasi, kitu ni kuvumilia. (uk. 5).

Kabla ya kufikia uamuzi kamili kuhusu suala hili likazuka suala lingine la uanakijiji - suala ambalo nafikiri ni la msingi pia. Baadhi ya wanakijiji walitaka waelezwe sifa za mwanakijiji. Hali ilivyo sasa hivi ni kuwa kuna uanakijiji wa aina mbili. Aina ya kwanza ni ile ya watu ambao wanaendesha maisha yao yote kijijini, na aina ya pili ni ile ya watu waishio mijini lakini wamejiandikisha katika vijiji na kutoa michango, halafu kwa michango hiyo wananunua haki zote za uanakijiji. Ni aina hii ya pili iletayo mgogoro na wanakijiji wanadahili uhalali wake.

*MWANAMKE I:* Zaidi kuna jambo ambalo limenikera siku nyingi sana ambalo Kamati yetu inaelekea kuridhika nalo. Kuna watu wanaokaa nje ya kijiji hiki - wengine mjini kabisa. Wengine wako Dar es Salaam. Sikuwa nafahamu kuwa watu hawa wanaitwa wanakijiji wa hapa mpaka wiki iliyopita wakati tunagawana faida ya mwaka. Wao walifika kuchukua faida yao na kuondoka. Wengine walipelekewa. Wengi tulistushwa na jambo hili. Itawezekanaje watu wasioishi kijijini wawe wanakijiji. Tulipouliza tukaelezwa kuwa eti wanaleta fedha. Ah! fedha. Kwa hiyo unaweza kununua uanakijiji! Lakini tukitazama vizuri tutaona kuwa hawa wanatununua sisi. Ni sawa na kuwafanyia kazi wao... (uk. 11).

Yote haya ni katika jumla ya matatizo yanayowakabili wanavijiji. Hususa hili la wanakijiji wa nje ni tatizo ambalo lingeweza kuepukwa kwa kuwakataa mpaka hatua za mbele za maendeleo ya vijiji. Hata hivyo wanakijiji wanaona kuwa hawa wanakijiji wa nje wafukuzwe kwanza kabla ya kufikiria matatizo ya wanakijiji "halisi."

*MTU I:* "Tatizo letu kubwa hapa ni mfarakano wetu wenyewe... Mara ngapi tumesema wasioishi kijijini si wanakijiji. Lakini badala yake viongozi wetu wanakubali hongo na kuwapokea watu hao kama wanakijiji kwa fedha. **(uk. 36)**

Kama ilivyoonekana huko nyuma msingi mkubwa wa matatizo ya vijiji vyetu ni uongozi mbaya. Viongozi ndio ambao wana kauli ya mwisho kuhusu lipi lifanywe na lipi lisifanywe na mara nyingi uamuzi wao hautokani na hima ya kulinda

masilahi ya wanakijiji kwa jumla bali yao wenyewe. Sikiliza anavyosema kiongozi huyu Makamu: "Fedha ndugu zinahitajika sana. Hatuwezi kufanya lolote bila fedha. Fedha ndiyo msingi wa kuanzishia kitu chochote."

Kauli hii ina upungufu wa namna mbili. Kwanza viongozi wa vijiji vyetu bado wanaona kuwa hawawezi kuendesha miradi muhimu inayohusiana na maendeleo ya vijiji bila ya kuwa na mtaji-fedha. Hili ni kosa maana nia kubwa ya vijiji ni kushawishi (*mobilize*) watu wafanye kazi zao za kila siku kwa bidii na juhudi zaidi kwa kutumia mbinu mpya na za kisasa ili kuweza kuleta mafanikio zaidi. Pili, kutokana na upungufu huo viongozi wameviingiza vijiji katika utumwa wa ubepari, kwani kutamani sana kitu usicho nacho kunaweza kukakuletea hali ya kumwenzi yule aliye nacho na kumpiga pambaja makusudi ya kuweko kwa vijiji.

3. UJAMAA NA NDOA

Katika kufikiria kuwafukuza wavivu, limezuka suala la ndoa. Ingawa Kizito ni mvivu na hatakiwi kijijini, lakini Kizito ni mtu mwenye mke. Je anapofukuzwa Kizito kijiji kitakuwa tayari kumfukuza mkewe pia alihali mkewe si mvivu? Na ikiwa Kizito atafukuzwa peke yake, kijiji kitakuwa tayari kubeba jukumu la kuivunja ndoa ya Kizito?

*BI KIZITO:* Lakini ikiwa mnataka tuwafukuze katika kijiji nataka mniambie, mimi je nitafukuzwa vilevile! Wasemaji wa kwanza wanasahau kuwa mnaowafukuza hawaishi peke yao. Wanawake na watoto. Je anayefukuzwa ni nani? Bwana peke yake au ukoo mzima nao utafukuzwa? (uk. 10)

Tatizo hili hakuliona Bibi Kizito peke yake bali hata wanakijiji wengine pia. Mtu hawezi kuwa amekamilika bila ya mwenzi wake na endapo itabidi watengane, wote wataumia kimaisha.

*MWANAMKE 1:* Nyinyi ndiyo mnaochanganya kila kitu na siasa. Bibi Kizito pia hivyo hivyo. Siasa ya ujamaa basi tena. Anaona hana haja ya mume. Huku ni kujidanganya. Hakuna mwanamke atakayeweza kuishi bila mume. (uk. 29).

Hili ni tatizo halisi ambalo linakabili vijiji vyetu na lisipoendewa vyema kuna hatari kubwa kwa watu kufikiria kuwa vijiji vya ujamaa huvunja ndoa za watu; na ndoa kama tujuavyo si kitu ambacho kila mtu au kikundi cha watu waweza kukiingilia.

*KIZITO:* Nataka Mwenyekiti anieleze sababu ya kunyang'anywa mke wangu. Mmempa kichwa mke wangu ili anichukie. Mnanitaka niondoke nimwache mke wangu. (uk. 38).

Matatizo yote haya yanazidi kusisitiza jambo moja kuwa kuna haja kubwa ya kuvumiliana kuonyana, kukumbushana na kuelimishana kwa kupeana ukweli ulivyo ili kuepuka matangukano kama haya. Na endapo hakuna mafanikio basi, mpaka hapo ndoa itaposhushwa hadhi yake. Kijiji hakina budi kukubali kuwafukuza wote ili kusalimisha ndoa, maana hata hapo zamani, endapo mmoja kati ya mtu mume na mkewe ataonekana na dosari na akaonekana kuwa hatakiwi, basi uamuzi ulikuwa kuwaamuru wote wahame bila ya kufikiria wema wa mmoja kati yao.

*MZEE 1:* Mlipoamua kumfukuza Kizito mngesema wazi wote wawili waondoke. Hamwezi kuwatenganisha watu wawili waliokuwa kitu kimoja. (uk. 37).

Yaelekea kuwa kauli ya Ngahyoma ya ushauri inaonekana katika wahusika Pinduo, Mzee 1 na Mwanamke 1. Kwa kumtumia Pinduo Ngahyoma anasema ni lazima wananchi wawe macho na kila wanapoona dosari yoyote ile katika viongozi au wanakijiji wawe tayari kuionyesha na kuisahihisha.

> *PINDUO:* "... Tumekataa ubwana lakini bado tunauruhusu ubwana. Twaambiwa: 'Hakuna ujamaa bila kazi ...' Lakini bado tunaruhusu watu wasiofanya kazi kupata ziada sawa nasi. Lakini ulipoanza kupotoshwa hakuna hata mmoja aliyejitokeza, akakunja ngumi na kupiga moyo konde kusema 'HAPANA ... KUNA WATU WANATUPOTOSHA." (uk. 20—21),

Akifafanua zaidi Pinduo anasema hivi:
Kwa nini watu tuendelee kuwa waoga wa kumwambia we! vitendo vyako havituridhishi. Wote tunaimba ujamaa lakini tunasahau adui tuliye naye hapa hapa. (uk. 40).

Matatizo ya uongozi yanamea katika vijiji kwa kuwa wanavijiji wanagwaya mbele ya viongozi, na kwa kweli hata katika sehemu nyingine pia. Na endapo tutafikia wakati wa kufuata mwito autoao Pinduo, sehemu kubwa ya matatizo ya kiutekelezaji yatapungua. Maana hivi sasa wanaongozwa wanakaribia viongozi wao kutokana na yale maagano ya mwanasimba na mbaa lakini simba bado kauvaa "usimba" wake?
Kwa kutumia Mzee 1 Ngahyoma anasema kuwa ili tutokwe na matatizo haya yanayotukabili viongozi washuke kwenye majukwaa waende shambani wakalime na kushiriki dhiki na harubu zote zinazowakabili wananchi. *Viongozi waache kusuku lugha ya kunata katika mabuku bali waukabili mpini, plao na kadhalika. Washiriki katika uzalishaji mali kwa vitendo.*

> *MZEE 1*: Ujamaa mpya mwingi ni wa kwenye vitabu. Na hatari yake ni kama hii. (Akionyesha mdomo). Maneno mengi na mikutano kila siku bila vitendo... Ingawa babu zetu hawakujirundika kama sisi (lakini) walikuwa wakiishi kijamaa kuliko sisi. Ujamaa ulikuwa ni maisha yao. (uk. 13).

Hii ina maana kuwa katika kuweka misingi ya ujamaa huu tulio nao hivi leo tulitegemea sana nadharia za vitabu. Hili ililikuwa kosa kubwa maana ni kweli kwamba shughuli za kushirikiana katika mambo mbalimbali katika jamii zilikuwapo lakini haielekei kuwa sisi tuliotekeleza tuliyazingatia. Ni kweli jamii nyingi zilikuwa na utaratibu wa kilimo lakini taratibu hizi hazikutumika katika kuwashawishi watu wainue hali zao. Kwa mfano, ikiwa jamii inafahamu *kiwili* ni nini na wataalamu wamekifanyia utafiti wa kutosha, *kiwili* hiki kingekuwa msingi wa kujenga vijiji. Watu wangesisitiziwa kukitumia *kiwili* ili kuhakikisha kuwa kila mmoja anapata shamba la kumtosha. Hatimaye isingekuwa taabu kuwashauri watu hao kuweka mashamba yao karibu karibu kwa urahisi wa kuendesha *kiwili.* Hizo zingekuwa hatua za vitendo kuelekea kwenye lengo letu. Maana tukiutumia vizuri utamaduni hatuwezi kupata matatizo makubwa katika miradi yetu.

> *MZEE 1:* Sisi tulizaliwa katika ujamaa. Tukakua katika ujamaa mpaka tuiipobughudhiwa na kuingiliwa na wakoloni kwa kutawaliwa. Maisha nayo yakabadilika, mila nazo zikabadilika ingawa si sana. (uk. 12—13).

Hali kadhalika Ngahyoma, japo hasemi moja kwa moja lakini aelekea kufikiri kuwa suala la ndoa si mchezo bali liangaliwe kwa uzito zaidi. Ndiyo maana kwa kumtumia mwanamke 1 Ngahyoma anasema:-

*Mwanamke 1:* (akiingia na kuwastua) na ukitazama sana Kizito ana haki ya kudai mke wake. (uk. 27).

Na ikiwa hapana budi watengane basi hapana shaka wote wataumia:

*MWANAMKE 1:* Wote wataumia, tayari Kizito ameanza kuona taabu ya kukosa jiko, kuona ukiwa na... Ndiyo maana anakazana kumtazama na kumtupia macho. Sasa hivi atapoteza heshima yake bure. (uk. 29).

Kwa ufupi hapa kuna tatizo ambalo labda yabidi sisi sote tulijadili wanaume peke yao na wanawake peke yao halafu matokeo ya pande mbili hizo yaletwe na kupambanishwa ili *izaliwe kauli moja maana ujamaa ni wetu na ndoa nazo ni zetu.* Je tutavitumikia vipi vitu viwili hivi bila kugongana? Suala hili limeanza kumkera Bibi Kizito. Anajiuliza anatafuta jibu. Hebu tumsikilize anavyosema:

*BI KIZITO:* Sijui... Labda kuna ukweli. Lakini upande mmoja kuna *Mume* na mwingine kuna *Ujamaa.* Yote ni maisha (Wanatoka). Lakini.... Lakini... (uk. 18).

Mimi sijui atakayeikamilisha sentensi inayomshinda Bi. Kizito! Sisi sote tunawajibika kulifikiria kwa makini zaidi suala hili maana kwa vyovyote ndege atakavyoruka atahitaji kitawi atue. Je kama kitawi hicho kikikatwa?